

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Rukwa
17 Julai, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemuagiza Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe kuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi wa Chakula (NFRA) ianze kununua mahindi kwa wakulima kote nchini kwa bei ya shilingi 700 kwa kilo nyongeza kutoka bei ya awali ya shilingi 500 kwa kilo iliyokuwepo wakati msimu wa ununuzi unaanza.

Rais Dkt. Samia ametoa agizo hilo leo wakati akihitimisha ziara yake mkoani humo kwa kuhutubia wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa CCM Mandela, Sumbawanga Mjini.

Aidha, Rais Dkt. Samia amewataka wananchi wa Rukwa wauze mazao ya kilimo kwa watu na taasisi ambazo zina vibali halali za kufanya biashara hiyo kutoka Wizara ya Kilimo ikiwemo vibali vya kuuza mahindi nje ya nchi.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amesema Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa meli na kuongeza meli mpya katika ziwa hilo.

Serikali imetoa boti nne za kisasa katika Ziwa Rukwa na Tanganyika ili zisaidie kuweka usalama ndani ya ziwa na kufanya shughuli za uvuvi wa kisasa.

Awali Rais Dkt. Samia aliweka Jiwe la Msingi ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya mkoa wa Rukwa iliyopo kijiji cha Mtindilo Laela ambapo amewataka wanafunzi kote nchini kuongeza bidii ya kujiendeleza katika masomo ya sayansi ili kupata wanafunzi wenye vipaji.

Rais Dkt. Samia pia alitembelea na kuzungumza na wanafunzi na Mapadri wa Shule ya Sekondari ya Seminari ya Kaengesa kabla yakuweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa Barabara ya lami ya Kaengesa.

Akiweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi ya Rukwa, Rais Samia amesema mradi huo utaleta mapinduzi katika elimu ya juu ambapo utawasaidia vijana kupata mafunzo kwa vitendo ambavyo vitawawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

